JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA

TANGAZO KWA WADAU WOTE WA TASNIA YA KOROSHO NCHINI

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) inapenda kuwataarifu wadau wote wa Tasnia ya Korosho nchini kwamba usafirishaji wa Korosho ghafi kutoka ghala za mnada kwenda Bandari ya Mtwara au katika ghala za wanunuzi za kuhifadhia Korosho utafanyika kwa muda wa saa 24. Ruhusa hii maalum imetolewa na Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Daniel Chongolo kwa ajili ya:-

i. Kuchukua tahadhari ya hali ya hewa iliyotolewa na TMA kwa kupunguza mlundikano wa korosho ghafi ghala za mnada ili kuruhusu korosho kutoka vyama vya msingi kuingia ghalani kwa wakati;
ii. Kuongeza mzunguko wa malori yaliyopo katika kusafirisha korosho ili kupunguza changamoto ya uhaba wa magari; na
iii. Kuwawezesha wanunuzi kuwahi Meli katika Bandari ya Mtwara.

Aidha, ruhusa hii imetolewa kwa Korosho zinazosafirishwa kutoka ghala kuu zilizopo mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma kwenda Bandari ya Mtwara au katika ghala za kuhifadhia Korosho zilizopo Mtwara. Hata hivyo ili kuongeza udhibiti wa ubora wa korosho usafirishaji wa korosho ghafi kutoka kwenye vyama ya msingi (AMCOS) Kwenda Ghala za mnada utaendelea kufanyika kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni. Aidha usafirishaji wa korosho kutoka mkoa wa Pwani na mikoa mingine kwenda bandari ya Dar es salaam utafanyika kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 12 jioni kama ilivyo katika **Mwongozo Na.1 wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho Ghafi kupitia Stakabadhi Ghalani Msimu wa 2026/2027 toleo la 6.**

Imetolewa na:
MKURUGENZI MKUU
BODI YA KOROSHO TANZANIA
30 October 2026

Korosho Marathon
Eat Cashew, Be healthy

EAT CASHEW
BE HEALTHY